# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO

# Jarida la Robo ya Tatu ya Mwaka

## (Aprili - Juni)

**Toleo Na. 0004**
**14, Julai 2023**



## Tufuatilie:

Chamwino Dc
Chamwino_dc
www.chamwinodc.go.tz
1126 Chamwino, Dodoma, Tanzania

#KAZI IENDELEE

# Yaliyomo


3 Chamwino Yapongezwa Kwakupata Hati Safi

4 Wizara ya Maliasili na Utalii na Chamwino Wapitisha Mpango wa Kanda wa Usimamizi wa Rasilimali

6 Uhamasishaji wa Matumizi ya Matokeo ya Sensa ya watu na Makazi ya Mwaka 2022

8 Naibu Wazri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Ashiriki Zoezi la upandaji Miti Chamwino

9 Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Akagua Miradi Chamwino

14 Waziri Kairuki Azindua Huduma Kituo cha Afya Dabalo



BODI YA WAHARIRI
Modesta Simon

# Chamwino Yapongezwa Kwakupata Hati Safi




Mkuu wa mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Staki Senyamule leo Julai 6, 2023 ameipomgeza Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kwa kupata Hati safi kwa hesabu za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo imeipa heshima Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino pamoja na Mkoa wa Dodoma.

Pongezi hizo amezitoa kwenye kikao maalum cha Balaza la Madiwani cha kupitia majibu ya hoja hizo kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashauri.

"Hongereni sana Chamwino ninaamini matokeo haya yanatokana nà ushirikiano chànya uliopo kati yenu Wahe. Madiwani, watendaji wa Halmashauri, viongozi na wadau mbalimbali wa Halmashauri husika. Hivyo nawasihi endeleeni kidumisha uhusiano huo ili kuendelea kuiwezesha Halmashauri ya chamwino kuendelea kupata hati safi kwenye kaguzi zote kama ambavyo imekuwa utamaduni wenu" Alisema Mkuu wa Mkoa.

Sambamba na pongezi hizo Mkuu wa Mkoa amewataka wataalam kuhakikisha hoja zote zilizobaki kufikia Julai 30 zinapatiwa majibu.

Aidha Mhe. Senyamule pia àmeipongeza Halmashauri katika ukusanyaji wa mapato kwa kuvuka lengo. Vilevile ametumia kikao hicho kutoa maelekezo mbalimbali kwa watendaji ikiwemo suala la ukusanyaji wa mapato na utengaji wa 10% za wanawake, vijana na walemavu. Vilevile kutenga fedha 40% kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Vilevile amewaekekeza Wakuu wa Idara za maendeleo ya jamii na Kilimo kushirikiana kwa pa,oja kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutunza chakula ili kuepukana na tatizo la njaa.

Kuhusu suala la mazingira ameelekeza kila kta kuhakikisha inaotesha kitalu cha miche ya miti kuanzia mwezi huu wa julai kwaajili ya kuipanda kipindi cha mvua kitakapofika.

Sambamba na hilo amemwelekeza Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya jamii kushirikiana na Afisa Afya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuwa na vyoo vya kudumu.

Katika kikao hicho Mkuu wa mkoa amemshukuru Mhe. Rais Samia Suluhu Hassani kwaFedha nyingi ambazo amezitoa kwenye Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo imeleta manufaa makubwa kwa wananchi.

# Wizara ya Maliasili na Utalii na Chamwino Wapitisha Mpango wa Kanda wa Usimamizi wa Rasilimali



Wizara ya Maliasili na utalii kwa Kushirikiana na Halmashauri.ya Wilaya ya Chamwino wamefanya kikao cha kupitisha Mpango wa Kanda wa Usimamizi wa Rasilimali (RZMP) Julai3, 2023. Kikao kimefanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashauri hiyo.

Baada ya kupata maoni ya wadau na kupitisha Mpango wa Kanda wa Usimamizi wa Rasilimali utawezesha eneo hilo kutangazwa kuwa Jumuiya ya Hifadhi na kupewa Haki ya Matumizi ya Rasilimali na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Wizara ya Maliasili na utalii kwa kushirikiana na Halmashauri ya wilaya ya Chamwino inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kupambana na ujangili na uthibiti biashara haramu ya nyara katika maeneo ya mfumo wa ikolojia wa Ruaha - Rungwa.

Vijiji vya Ndogowe na Mlazo wamefanikiwa kuanzisha Hifadhi ya wanyamapori Jamii - Wildlife Management Area- WMA inayopakana na maeneo ya Hifadhi hasa hifadhi ya wanyamapori MBOMIPA - IRINGA. Vijiji hivi ni katiya vijiji 10 vya Tarafa ya Mpwayungu vinavyokabiliana na changamoto wanyamapori wakali na waharibifu.

Akizungumza alipokuwa akifungua kikao hicho Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Chamwino Dkt. Semistatus H. Mashimba amipongeza Wizara ya Maliasili na utalii kwa kufanikiwa kuanzisha WMA pamoja na wananchi waliokubali kuanzisha. Alimuahidi Mkurugenzi kutoka wizara ya Maliasili Dkt. Msofe kuwa watahakikisha na vijiji 8 ambavyo bado havijajiunga vinajiunga na mradi huo.

“Tutahakikisha vijiji 8 ambavyo havijajiunga na mpango huo vinajiunga. Tutashirikiana kutoa elimu na nadhani kwa muda mfupi sana hao waliojiunga watakuwa mfano wa kusababisha wenzetu kutafakari upya na kujiunga na mradi huu.” Alisema Dkt. Mashimba.

Aidha alieleza kuwa mradi umelenga kuwawezesha wananchi kupata manufaa kupitia wanyamapori kwenye vijiji vyao ambavyo vimekuwa vikikabiliwa na wanyamapori wakali na waharibifu hususani kwenye mazao na kusababisha hasara



kubwa kwa wananchi.

Alieleza pia ili kuwezesha wananchi kufaidika na rasilimali za wanyamapori sheria imeelekeza kuanziasha WMA ili wananchi waweze kupata haki za matumizi ya rasilimali zote zinazowazunguka.

“Natumia fursa hii kuipongeza Wizara ya Maliasili na utalii kwa uwezeshaji wa mradi huu katika wilaya yetu ya Chamwino, aidha nawapongeza na viongozi wote wa Kata, Tarafa, vijiji na Wilaya kwa kuhakikisha mradi huu unakwenda kutelezwa vizuri.” Alisema Dkt. Mashimba.

“ Uwepo wa maeneo haya yanasaidia shughuli zote za kimila na kitamaduni kupata fursa kubwa kwa wawekezaji, hivyo ninawasihi sana viongozi wote na wananchiwa Wilaya tuendwlee kushirikiana ili kuwezeaha kufanikisha mirasi ya wizara hii, hususqni huu utekelezeke vizuri na tuhakikishe tunapata mafanikio makubwa kwenye Halmashauri yetu.” Alisema Dkt. Mashimba.

Aliwaomba wananchi wanaporudi kwenye maeneo yao wasigeuke kuwa vikwazo vya kukwamisha mradi huu.

# Uhamasishaji wa Matumizi ya Matokeo ya Sensa ya watu na Makazi ya Mwaka 2022

Mkuu wa Wilaya ya Chamwino Mhe. Gifty Isaya Msuya, amewapongeza Ofisi ya Takwimu ya Taifa kwa kuwasilisha matokeo ya sensa kwa ngazi ya wilaya na kata.

Pongezi hizo amezitoa wakati wa uwasilishwaji na utoaji wa takwimu katika wilaya ya Chamwino iliyofanyika, 28 juni 2023 wilayani hapo.

"Niwapongeze kwa zoezi hili mmetoa ushirikiano zaidi kwa kufanikisha zoezi hili, ndugu zangu wanachamwaino niwaambie jambo moja sisi Chamwino na mkoa wa Dodoma tunabahati kubwa sana kwa sababu uzinduzi wa muongozo wa sensa umefanyika hapa Dodoma, lakini uzinduzi wa kwanza wa matokeo ya sensa Tanzania yamefanyika hapa Dodoma, lakini pia uwasilishaji wa namna hii ya kuwaita viongozi wote wa vijiji, kata mpaka chini imefanyika mkoa wa Dar es salaam na Dodoma,"



"Hii inaonyesha sasa tukae mguu sawa kwakuwa mambo mazuri yanakuja lakini niwaombe sana taarifa zilizotolewa za matokeo zinasema kwamba matokeo ya vijiji na vitongoji yamesha chakatwa lakini yanasubiri taratibu ya kuzinduliwa na kutumika", alisema Mkuu wa Wilaya.




Kwa sasa wilaya ya Chamwino kwa mujibu wa takwimu za sensa ya watu na makazi ya 2022 inajumla ya idadi ya watu 486,176

# Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Akagua Mirdi ya Maendeleo Chamwino

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Rosemary Staki Senyamule amefanya ziara ya kukagua miradi ya ujenzi wa madarasa yanayojengwa kwa fedha za mradi wa Boost.

Ukaguzi huo umefanyika Mei 30, 2023 kwenye kata za Handali kijiji cha mjeloo ambapo inajengwa shule nzima yenye mikondo miwili na kata ya Makang'wa kijiji cha Makang'wa ambapo yanajengwa madarasa nane.

Akizungumza na wananchi Mkuu wa Mkoa amewahimiza kuchangia nguvu kazi kuunga juhudi za Serikali kama walivyokubaliana kwani kwa kufanya hivyo wataweza kupata fedha ya ziada ambayo inaweza kufanya kazi nyingine ya maendeleo kwenye shule zao.

"Nawasihi wananchi kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kuchangia maendeleo kwani hayana mwisho na wala hakuna mwisho wa kufanya kazi hivyo mjitume"

Akiwa Handal amepongeza kwa hatua ya ujenzi iliyofikiwa na amewahimiza mafundi kufanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha ujenzi wa madarasa hayo kwani yanatakiwa kukamilika na kukabidhiwa kwake ifikapo Juni 20, 2023 na wizarani majengo yanapaswa kukabidhiwa Juni 30, 2023.



Aidha mkuu wa Mkoa amefanya mkutano wa hadhara ambapo amepokea na kujibu kero mbalimbali za wananchi

Vilevile Mkuu wa Mkoa amempongeza na kumshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hasan kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwapelekea wananchi maendeleo na amewaomba wananchi kuendelea kuyatangaza mazuri hayo.

# Naibu Wazri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Ashiriki Zoezi la upandaji Miti Chamwino



Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Khamis Hamza Khamis ameongoza zoezi la upandaji miti lililofanyika leo Mei 26, 2023 shule ya sekondari Buigiri.

Taasis zilizohisani zoezi hili ni TCCHP ikishirikiana na Habari Conservation Chini ya ufadhili wa TFS - PMM Living way.

Akizungumza nawananchi Mhe. Khamis Hamza Hamis amewahimiza wadau wote wa mazingira hususani waandishi wa habari kuendelea kutoa elimu ya mazingira.

" Wanahabari tumieni weledi wenu kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kutunza mazingira na athari zake," alisema.

Vilevile aliendelea kusema kuwa ipo haja ya kuendelea kutoa elimu ya kuepuka mabadiliko ya tabia ya nchi kwa kuunga juhudi za Serikali.

" Tupandeni miti mingi na kuitunza, tumeshazindua kampeni maalum mashuleni ya kusomana kupanda miti." Alisema Naibu Waziri.

Aidha Naibu Waziri alizungumzia kuhusu suala la biashara ya hewa ukaa ambapo alieleza kuwa bado jamii haijawa na uelewa juu yake na kuelekeza kuwa elimu iendelee kutolewa kuhusiana na biashara hiyo.

"Biashara ya hewa ukaa, bado jamii haijajua taaluma hii, hivyo naomba mkawape taaluma wananchi wetu, moja namna ya kujua fursa na namna gani ya kunufaika na biashara hii na watu wa habari mnayo nafasi kubwa ya kuelimisha jamii," alisema Naibu Waziri.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na mazingira alizungumzia suala la uelewa mdogo wa wananchi katika kutunza vyanzo vya maji na kueleza kuwa hakuna mazingira bila maji, na ndio maana siku hizi wanashuhudia wanyama wakitangatanga kwenye makazi ya watu wakitafuta maji. Alielekeza shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji kama vile kilimo, kunywesha mifugo na uchimbaji madini zidhibitiwe.

Vilevile alizungumzia suala la kuwasaidia watu wenye ulemavu hususani wenye ulemavu wa ngozi ( ualbino) pamoja na viungo kwa kupanda miti kwa maana wanapata tabu na jua kali.

Jumla ya miti 1,000 imepandwa ambapo miti ya matunda ni 700 na ya kivuli 300. Mhe. Naibu Waziri amesisitiza miti hiyo itunzwe vizuri ili ikue.



# Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma Akagua Miradi Chamwino

Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Ally Gugu amewataka viongozi Wilayani Chamwino kutekeleza miradi kwa wakati na na kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa kwenye miradi hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa wakati wa ziara ya kukagua baadhi ya miradi inayotekelezwa katika Halmasahauri ya Wilaya ya Chamwino, tarehe Mei 05, 2023, na alipata nafasi kuzungumza na watumishi wa wilaya hiyo kwa lengo la kuweka mikakati bora ya utendaji kazi ili kufikia malengo ya maendeleo kwa uharaka.

"Tumebaini baadhi ya maeneo ambayo yamefanyika vizuri lakini yapo maeneo ambayo yanahitaji kuimarishwa. lakini angalizo

Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Ally Gugu amewataka viongozi Wilayani Chamwino kutekeleza miradi kwa wakati na na kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa kwenye miradi hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa wakati wa ziara ya kukagua baadhi ya miradi inayotekelezwa katika Halmasahauri ya Wilaya ya Chamwino, tarehe Mei 05, 2023, na alipata nafasi kuzungumza na watumishi wa wilaya hiyo kwa lengo la kuweka mikakati bora ya utendaji kazi ili kufikia malengo ya maendeleo kwa uharaka.

"Tumebaini baadhi ya maeneo ambayo yamefanyika vizuri lakini yapo maeneo ambayo yanahitaji kuimarishwa. lakini angalizo kwenye maeneo yaliyobaki ya ujenzi basi tuzingatie yafanyike kwa umahiri zaidi lakini jengoi lizingatie viwango vya juu vya kupendeza." Alisema Gugu.



Aidha Gugu ameipongeza Halmashauri kwa juhudi za utekelezaji wa miradi mbalimbali kupitia mapato ya ndani ikiwemo Zahanati ya Kijiji cha Wilunze ambapo ujenzi umefikia hatua ya umaliziaji.

"Kutokana na mapato ya ndani wenzetu wa Halmashauri waliweza kutenga fedha ambazo zimewezesha kuwa na jengo ambalo tayari tumejiridhisha liko kwenye hatua nzuri sana, na hivyo wahakikishe kazi inayoendelea isimamiwe ipasavyo hata umaliziaji wa jengo hili uweze kufanyika vizuri,"

Aidha Katibu Tawala Mkoa alieleza kuwa mradi huu wa zahanati ulikuwa katika miradi ambayo ya mwaka wa fedha 2021/2022 kwa hiyo tumeona upo nyuma na hivyo tulikubaliana tuhakikishe mradi huo unaanza kutoa huduma kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha yaani tarehe 30, juni 2023.

Hata hivyo Gugu amesisitiza miradi inayotekelezwa kwa fedha za boost inapaswa kukamilishwa kwa wakati ifikapo juni 30, mwaka huu.

Katika ziara hiyo Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma alikagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Zahanati ya Kijiji cha Wilunze ambavyo ujenzi wake unaendele na Mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya maabara ya baiolojioa na kemia katika shule ya sekondari msanga ambapo mradi upo hatua ya umaliziaji.

# Mkuu wa Wilaya Chamwino na Viongozi wa Halmashauri Wakagua Maendeleo ya Ujenzi Mradi wa Boost



Mkuu wa Wilaya ya Chamwino Mhe. Gifty Isaya Msuya, 15 Mei 2023 amekagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa shule ya msingi mpya yenye mikondo miwili inayojengwa katika kijiji cha Mjelo, unaotekelezwa kwa fedha za mradi wa Boost.

Mhe. Gifty amesema shule hiyo ilikuwa ni shule shikizi iliyojengwa kwa nguvu za wananchi kwa kujenga darasa la awali na darasa la kwanza .

Hata hivyo ameishukuru Serikali ya awamu ya sita kwa kukipatia kijiji hicho kiasi cha fedha shilingi milioni 490 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 14, ofisi ya utawala na matundu 24 ya vyoo.

"Ndugu zangu wa Mjelo sisi tumekuja kuangalia maendeleo ya mradi ni dhahiri kwamba tangu kipindi cha Uhuru miaka 60 ya Uhuru iliyopita ambapo kijiji hiki kilikuwa kimoja cha Handali na baadae tukagawanyika na kupata Mjelo na Handali, lakini kwa kipindi tangu mimi nimefika kumekuwa na malalamiko kwamba shule ya msingi Handali imeelemewa inawanafunzi wengi, majengo machache, lakini eneo pia ni dogo na malalamiko haya tumekuwa tukipokea kupitia vikao mbalimbali."

"Nimeambiwa hapa kuna shule shikizi darasa la awali na darasa la kwanza ambao wanasomea hapa na sisi tukaona katika utaratibu huu ambao Mhe. Rais ametoa fedha nyingi za kujenga madarasa tukaomba kupitia Mbunge wenu, viongozi wa kata, Waheshimiwa Madiwani, wakawasilisha maombi kwamba tupatiwe shule nyingine pacha na sisi tukaona ni wazo zuri, tukaomba fedha hizi TAMISEMI natukafanikiwa kupata milioni 490 katika eneo hili ambapo yatajengwa madarasa 14, ofisi ya utawala, na matundu 24 ya vyoo ", alisema Mkuu wa Wilaya.



viongozi wa kata, Waheshimiwa Madiwani, wakawasilisha maombi kwamba tupatiwe shule nyingine pacha na sisi tukaona ni wazo zuri, tukaomba fedha hizi TAMISEMI natukafanikiwa kupata milioni 490 katika eneo hili ambapo yatajengwa madarasa 14, ofisi ya utawala, na matundu 24 ya vyoo ", alisema Mkuu wa Wilaya.

Vilevile Mhe. Gifty amewasisitiza wananchi kushiriki katika utekelezaji wa miradi hiyo kwa kujitolea nguvu kazi ili kuhakikisha miundombinu inajengwa kwa ukamilifu.

Alisema wanachi watakaposhiriki itasaidia kuhifadhi fedha nyingine kwaajili ya kukarabati madarasa ambayo yalijengwa kwa nguvu za wananchi.

"Sasa Serikali ya Mhe. Samia Suluhu Hassani inatoa mabilioni lakini katika kutoa fedha hizi haitaki wanachi wabaki nyuma lazima wananchi wajue kinachoendelea lakini washiriki moja kwa moja kwenye kuhakikisha miundombinu hii inajengwa kwa ukamilifu, lakini fedha inayotumika inatumika vizuri na nguvu kazi inatakiwa wananchi wachimbe msingi, wakusanye kokoto, mawe na bahati nzuri tumejaliwa mchanga huku Handali na Mjelo, tukusanye mchanga ili tupunguze gharama za mradi,"

" Inaonekana hapa wanchi kujitoa ni shida, kwa hiyo wananchi mnapaswa kujitoa ili shule yetu iwe ya mfano. Lazima zifanane isiwe kule kuna madarasa mazuri huku kuna magofu haitopendeza. Tunahitajika tutoe nguvu kazi ili tusiweke hela nyingi kwenye hizi kazi ambazo tunaweza kufanya kwa mikono yetu, ili pesa zielekezwe kwenye vitu vinavyotoka viwandani zaidi." Alisema.



# Chamwino Yatoa Vyeti Vya Pongezi Kwa NGO's



Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imetoa vyeti vya pongezi kwa NGO's zinazofanya kazi wilayani humo ikiwa na lengo la kutambua mchango unaotolewa na NGO's hizo.

Vyeti hivyo vimetolewa leo kwenye kikao cha tathimini ya utendaji kazi wa mashirika hayo Mei 12, 2023 kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashauri.

Jumla ya NGO's15 zilikabidhiwa vyeti kwa vigezo mbalimbali kulingana na huduma wanazozitoa kwa jamii ya Chamwino.

NGO's ni pamoja na Katuka paralegal, Tayoa, Black Maendeleo Tanzania,EGPAF, Water Mission, Development services coordination, Innovation of Africa, Sustainable Agriculture Tanzania, SAT uwezeshaji wanawake, Children in cross fire, Restless Development, Safe Island for women, Compaign for women and children Tanzania, Doctors with Africa(KUAMM), The lead Foundation na Lay Volunteer International Association.

Mgeni Rasmi kwenye kikao hicho alikuwa ni Mkuu wa Wilaya ya Chamwino Mhe. Gift Isaya Msuya ambaye aliwakilishwa na Katibu Tawala wa Wilaya Bi Neema Nyalega.

Katibu tawala amezisisitiza NGO's kuwasilisha taarifa zao za kila robo mwaka pamoja na taarifa za bajeti zao kwani zinasaidia Halmashauri kuweza kuweka mango mzuri wa kibajeti katika kutoa huduma kwa wananchi. " Nasisitiza kwa kila taasis isiyo ya Kiserikali kuhakikisha inawasilisha bajeti yake Halmashauri na jambo hili si la mzaha. Taasisi itakayoshindwa kuwasilisha bajeti hatua zitachukuliwa dhidi yake." Alisema.

# Waziri Kairuki Azindua Huduma Kituo cha Afya Dabalo

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Angellah Kairuki , amezindua jengo la upasuaji na wodi ya wazazi katika kituo cha afya Dabalo wakati wa hafla ya makabidhiano ya jengo la upasuaji, wodi ya wazazi, vifaa tiba , vifaa na gari la kubebea wagonjwa katika kituo hicho.




Akizungumza katika hafla hiyo mei 09, 2023, amesema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma bora za afya kwa kuwasogezea huduma hizo karibu na makazi yao.

“Ndugu zangu Mhe. Rais wetu kila mara anaendelea kupambana kuhakikisha anaendelea kukazania vipaumbele vyake, nchi yetu inamahitaji makubwa na mmeona ni kwa namna gani ndani ya muda mfupi ameendelea kuweka mkazo katika kushughulikia vipaumbele mablimbali ikiwemo kuweka huduma karibu na wananchi, ”Alisema Waziri Kairuki.

“Mmeona ni kwa namna gani kwa sekta ya Afya jinsi ambavyo ameweka kipaumbele katika utoaji wa huduma za afya lakini vilevile sio huduma tu pia kuhakikisha kwamba hata zile gharama zinazotozwa basi zinakuwa ni gharama ambazo kweli wananchi wetu wanaweza kuzimudu”, alisema.

Mhe. Angellah Kairuki amelishukuru shirika la Umoja wa Mataifa linaloshugulikia idadi ya watu duniani (UNFPA) kupitia mradi wa kuboresha huduma za afya ya uzazi , watoto na vijana (RMNCAH – UFPA) iliyofadhiliwa na serikali ya Denmark

“Nipende pia kuwashukuru shirika la Umoja wa Mataifa linaloshugulikia idadi ya watu duniani (UNFPA) kupitia mradi wa kuboresha huduma za afya ya uzazi , watoto na vijana (RMNCAH – UFPA) iliyofadhiliwa na Serikali ya Denmark kwa namna ambavyo wameendelea kutoa huduma mbalimbali na misaada katika sekta ya afya na sekta nyingine ,”alisema.

“Hii inaonyesha ni namna gani wanayo dhamira na wajibu wa kuendelea kushirikiana na kuunga mkono jitihada na juhudi mbalimbali za Serikali na hasa katika kuwafikia wananchi wetu wa Tanzania na hususani walio achwa nyuma na huduma bora za afya,” alisema Waziri Kairuki

# Kamati za Kudumu za Madiwani Chamwino Zapongezwa



Kamati ya Fedha, Utawala na Uongozi pamoja na kamati ya Elimu, Afya na maji Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino zimepongezwa kwa ukusanyaji mzuri wa Mapato na usimamizi mzuri wa huduma za afya na elimu.

Pongezi hizo zimetolewa na Wahe. Madiwani pamoja na Afisa kutoka Serikali za mitaa Mkoa wa Dodoma leo Mei 3, 2023 kwenye kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya tatu kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashauri.

Imeelezwa kuwa hadi sasa makusanyo yamefikia asilimia 83 ya lengo la makusanyo. Vilevile alielekeza kila shule na kila kata ianzishe vitalu vya miti na miche hiyo itakapokuwa tayari igawiwe kwenye taasis za Serikali ili ipandwe na kila kaya pia itapaswa kuapanda miti mitano na kuanzia mwezi wa tatu watapita kukagua.

Suala la shule kuwa chafu, alielekeza walimu wawasimamie wanafunzi kufanya usafi.

Suala la kusaini mikataba alieleza kuwa mkataba ni sheria hivyo kwa kushindwa kutekeleza yaliyomo kwenye mkataba watachukuliwa hatua. Aliendelea kueleza kuwa mitihani ya kila mwezi ndio itakayotumika kupima matokeo( performance appraisal) watakaofanya vizuri watapongezwa na watakaofanya vibaya watapewa bendera nyekundu wakapeperushe kwenye shule zao.

Aliwaomba wawe tayari kujifunza na kufanya mabadiliko. Vilevile wawe na utayari wa kupokea maelekezo ya viongozi. Wajifunze kwa wengine waliofanikiwa hawataonekana wajinga kwa kufanya hivyo.

Mkuu wa wilaya pia aliahidi kusimamia haki za walimu na watumishi wengine kama waziri wa TAMISEMI alivyoelekeza lakini alisisitiza haki iendane na wajibu.

Katika kikao hicho wajumbe walipitia na kujadili kuhusu mpango kazi wa Mkoa kuhusu elimu ya msingi pamoja na mpango mkakati maalum wa Wilaya kwa ajili ya darasa la saba.

# Kuelekea Miaka 59 ya Uhuru, Mhe. Senyamule Azindua Mradi wa Maji Buigiri



Kuelekea kilele cha Maadhimisho ya Miaka 59 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule amezindua mradi wa ujenzi wa tenki la maji lenye ujazo wa lita million 2.5 lililopo katika kata ya Buigiri wilaya ya chamwino.

Akizungumza katika uzinduzi huo alisema tarehe 26, Aprili kila mwaka wananchi husherekea maadhimisho hayo ambapo kwa mwaka huu yatafanyika kwa kila mkoa kwa mujibu wa maelekezo yaliyotelewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassani kupitia kwa Waziri mkuu Mhe Kasimu Majaliwa.

“Kila mwaka tumekuwa tukisheherekea siku hizi na mwaka huu tulipokea maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia kwa Wazitri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kasimu Majaliwa, akitoa maelekezo ya namna ambavyo nchi yetu itaadhimisha maadhimisho ya miaka 59 ya muungano”,

“Na maelekezo hayo yalitutaka tusherehekee kwa ngazi za mikoa na wilaya lakini maelekezo mengine yalitutaka tuendelee kuadhimisha kwa namna mbalimbali za kushirikisha wananchi, kufungua miradi, kuwa na makongamano na huduma mbalimbali za kuwaeleza watanzania wajuwe nini Muungano, faida zake ni nini na wapi tunaelekea katika Muungano wa nchi hizi mbili kwa hiyo leo tupo hapa ikiwa ni sehemu ya maadhimisho haya”, alisema Mhe Rosemary Senyemule.

Hata hivyo alisema wanachi wanapaswa kutunza, kuilinda na kuonyesha utashi kwenye utunzaji na utumiaji wa maji hayo kwa umakini na kuhakikisha miundo mbinu hiyo hayailiwi wala haichezewi.

Aidha ametoa wito kwa wanachi kulipa bili za maji ili kuendelea kuboresha na kuendeleza miundo mbinu ya upatikanaji wa maji na kupunguza kero zinazo patikana katika jamii.

“Nitoe wito kwa wananchi mnaoneda kutumia maji haya wengine wakisikia upatikanaji ni zaidi ya asilimia 100 wanasema sasa hata nikiacha bomba wazi hayatoisha, hapana maji ni bidhaa adimu maji yanatakiwa yaheshimiwe yatumike kwa umakini mkubwa”,

“Lakini jingine mlipe bili za maji lazima unapotumia maji kuhakikisha unalipia gharama ambazo zinatakiwa kuzirejesha ili uendeshaji wa miradi hizi ziwe endelevu”, alisema.

Chamwino Buigiri

Chamwino Dc

Chamwino_dc

www.chamwinodc.go.tz

S.L.P 1126 Dodoma